

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA**

**MKOA WA NJOMBE**

Anuani “Afya”

Nambari ya Simu +25526-2782912  
Nukushi. +225 – 262782914  
Email:mgangamfawidhi@njomberh.go.tz



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,  
14 Barabara ya Hospitali ya Rufaa,  
59107 Ramadhani - Njombe,  
S. L. P 1044,  
**NJOMBE.**

18, Novemba, 2024

**TAARIFA KWA UMMA**

**UWEPO WA KAMBI YA MADAKTARI BINGWA NA BOBEZI, HOSPITALI YA RUFAA YA  
MKOA WA NJOMBE KUANZIA DESEMBA 02 HADI DESEMBA 07, 2024**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe anawatangazia wananchi wa Mkoa wa Njombe na mikoa jirani kuwa kuanzia tarehe 02 Desemba hadi Desemba 7, 2024, kutakuwa na Kambi ya Madaktari Bingwa Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe, kwa kushirikiana na **Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili – Mirembe, Taasisi ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya** na Hospitali zote za Rufaa za Mikoa zilizopo Nyanda za Juu Kusini, ikijumuisha mikoa ya **Mbeya, Ruvuma, na Songwe** watakahohudumia wananchi wa mkoa huu wa Njombe na mikoa jirani.

Tunatarajia kuwa na wataalam katika nyanja mbalimbali za afya kama ifuatavyo:-

1. Daktari bingwa Bobezi wa Magonjwa ya Moyo (Cardiologist)
2. Daktari bingwa Bobezi wa magonjwa ya Figo (Nephrologist)
3. Daktari bingwa bobezi upasuaji Rekebishi (Plastic Surgeon)
4. Daktari bingwa bobezi upasuaji wa ubongo (Neurosurgeon)
5. Daktari bingwa Upasuaji wa Mfumo wa mkojo (Urologist)
6. Daktari bingwa wa magonjwa ya saratani (Oncologist)
7. Daktari bingwa matibabu na upasuaji wa Macho (Ophthalmologist)
8. Daktari bingwa afya ya akili (pyschiatrist)
9. Daktari bingwa matibabu na upasuaji wa Sikio, Pua na Koo (ENT Surgeon)
10. Daktari bingwa Upasuaji wa mifupa (Orthopaedic Surgeon)
11. Daktari bingwa Upasuaji wa Jumla (General Surgeon)
12. Daktari bingwa Upasuaji wa Kinywa na Meno (Maxillofacial surgeon)
13. Daktari Bingwa wa Watoto (Paediatrician)
14. Daktari bingwa Magonjwa ya Wanawake na uzazi (Obstetrician/Gynecologist)
15. Daktari bingwa Magonjwa ya Ndani (Physician)
16. Daktari Bingwa wa Dawa za Usingizi na Ganzi (Anesthesiologist)
17. Huduma za kibingwa kwa wagonjwa mahututi (critical care)
18. Huduma za Tiba ya viungo na utengamao (physiotherapy and rehabilitation)
19. Daktari bingwa wa ngozi (Dermatologist)
20. Daktari bingwa radiolojia (Radiologist)
21. Mtaalam wa usikivu (Audiologist)

Huduma zitatolewa kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni.

Lengo kubwa la uwepo wa Kambi hiyo ni kuendelea kutimiza adhma ya serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kusogezza/kufikisha huduma za Kibingwa na ubingwa Bobezi kwa wananchi katika maeneo yao.

Kwa taarifa hii wananchi wa mikoa ya Njombe, Ruvuma, Songwe na Mbeya, wenyewe changamoto mbalimbali za kiafya na wanatamani kukutana na wataalamu katika maeneo yaliyoainishwa mnaaswa kufika kwa ajili ya kukutana na wataalamu hao na kupata huduma hizo kwa tarehe zilizotajwa.Zoezi litahusisha gharama za uchangiaji na bima.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba hii



**Imetolewa na:** Ombeni S. Utembele  
**AFISA UHUSIANO**

**Kny: Mganga Mfawidhi**  
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe**